

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA

Simu: +255-22-2133964, 2133969
Barua Pepe: info@nhif.or.tz
Tovuti: www.nhif.or.tz
Nukushi: +255-22-2133972,
2133982



Makao Makuu
Kurasini Bendera Tatu
S.L.P. 11360, Dar es Salaam
Tanzania

TAARIFA KWA UMMA

UFAFANUZI WA MATUMIZI SAHIHI YA KADI ZA NHIF KUKANUSHA HABARI INAYOTAPAKAA KWENYE MITANDAO YA KIJAMII

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unapenda kutoa ufafanuzi juu ya habari zinazoendelea kusambazwa katika baadhi ya mitandao ya kijamii kuhusu uhalali wa mwanachama kutoa kadi yake ya NHIF kutumika na mtu mwingine. Hii ni baada ya makosa yaliyojitokeza kwenye taarifa iliyorushwa na televisheni ya Channel Ten kutoka Geita iliyodai Mkuu wa Wilaya hiyo kutoa kadi yake ya NHIF illi kutibia watu walioshambuliwa na fisi. Ufafanuzi wa suala hili ni kama ifuatavyo:-

1. Taarifa hii haikutolewa kwa usahihi na baada ya kugundua hilo, Mkuu wa Wilaya ya Geita alilitolea ufafanuzi na kueleza usahihi wa habari hiyo kupitia taarifa ya habari iliyorushwa na chombo hicho siku iliyofuata. Kulingana na ufafanuzi huo, Mkuu wa Wilaya ya Geita alilipa gharama za matibabu kwa majeruhi hao lakini pia aliwakatia kadi za Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na kuwahimiza wananchi kuwa na bima ya afya ili kuwa na uhakika wa matibabu endapo watapata dharula kama hizo.
2. NHIF inaendelea kuwakumbusha wanachama wake kuwa ni kosa la jinai kutumia kadi ya mtu mwingine au ya kughushi kupata huduma za matibabu.
3. Mfuko kwa kushirikiana na wadau wake unaendelea kubaini na kuwachukulia hatua za kisheria wote wanaopatikana na makosa hayo.

Aidha, Mfuko unachukua fursa hii kuwakumbusha watoa huduma waliosajiliwa na Mfuko kuhakiki uhalali wa kadi za wanachama kabla ya kutoa huduma

Mfuko unaendelea kuwahimiza wananchi kuwa endapo kuna suala lolote la Mfuko ambalo linahitaji ufafanuzi ni vema kuwasiliana na uongozi wa NHIF ili kupata ufafanuzi sahihi ili kuepuka taarifa zinazoweza leta mgongano katika jamii. Mfuko unathamini mrejesho kutoka kwa umma, hivyo wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja simu bila malipo 0800 110063 kwa taarifa zaidi. Mfuko unaomba radhi kwa usumbufu wowote uliojitokeza kwa wadau wake kutokana na taarifa hizo.

Imetolewa na;

MKURUGENZI MKUU
MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA
3 Disemba 2017